BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Tano – Tarehe 15 Septemba, 2026**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

50. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kumbukumbu zinaonesha kuwa Zanzibar imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu pamoja na utekelezaji wake. Kwa mnasaba huo, ninaipongeza Serikali kwa kuanza jitihada za kutengeneza Mfumo Jumuishi wa Kitaifa wa Data za Watu Wenye Ulemavu Zanzibar.

(a) Je, Mfumo huu umefikia wapi katika uundwaji wake na lini utakuwa tayari kwa matumizi.

(b) Je, Wizara imechukua jitihada gani kuhakikisha sekta zote za huduma na fursa zinazounganisha Mfumo huu katika Mifumo yao ili kurahisisha upatikanaji sawa, fursa na huduma kwa Watu Wenye Ulemavu.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

222. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika kipindi cha miezi kadhaa iliyopita, kulikuwa na picha iliyotembea mitandaoni ya Mwanafunzi wa Chuo cha Mafunzo, aliyetoroka na kupatikana baada ya kutafutwa, lakini Mwanafunzi huyo alionekana akiwa anapigwa kipigo cha kuumiza sana.

(a) Je, kwa kiasi gani vitendo vya kumpiga Mwanafunzi huyo vinakwenda kinyume na ni uvunjifu wa haki za binaadamu.

(b) Je, vikosi vyetu vina haki gani ya kumpiga na kumdhalilisha Mwanafunzi aliyejaribu kutoroka.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

217. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilikuwa na miradi mingi katika Wilaya ya Magharibi 'B'.

(a) Ni miradi mingapi imekamilika na mingapi haikukamilika katika Wilaya ya Magharibi 'B' kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

(b) Ni sababu zipi zilizopelekea kutokukamilika kwa miradi ya Wilaya ya Magharibi 'B' kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuikamilisha miradi iliyokuwa haijakamilika katika mwaka wa fedha uliopita, kupitia Wilaya ya Magharibi 'B'.

298. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Wananchi na wafanyabiashara wanalalamikia wingi wa kodi na tozo mbalimbali unaoongeza gharama za maisha na uendeshaji wa biashara.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini gani kuhusu athari za wingi wa kodi na tozo kwa wananchi na wafanyabiashara wadogo.

(b) Ni kodi na tozo zipi Serikali imebaini kuwa zinafanana au kumtoza mwananchi zaidi ya mara moja katika shughuli moja.

(c) Serikali ina mpango gani wa kupunguza au kuunganisha baadhi ya kodi na tozo ili kupunguza gharama za kufanya biashara Zanzibar.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

306. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Serikali iliamua kuvikodisha visiwa mbalimbali kwa Wawekezaji, ili kuiongezea mapato Serikali.

(a) Je, ni visiwa vingapi vimeanza utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

(b) Je, vile visiwa vilivyoshindwa ni vipi na kwa nini vimeshindwa kuwekezwa.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

41. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Miongoni mwa majengo makongwe yaliyopo katika Jimbo la Chake Chake ni jengo maarufu la JAN Building lililopo Kichungwani, ambalo kutokana na ukongwe wake limekuwa katika hali ya uchakavu, licha ya wananchi kuendelea kulitumia kwa makaazi.

Je, Serikali ina tathmini gani ya kitaalamu kuhusu hali ya usalama wa jengo hilo kwa matumizi ya wananchi wanaoishi humo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

133. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Baadhi ya bomba za maji safi za Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) zimepita ndani ya chemba (*man-hole*) za maji taka katika maeneo mbalimbali ya Mji Mkongwe na muda mwengine husababisha maji safi kuchanganyika na maji taka.

(a) Je, sababu gani zilizosababisha chemba za maji machafu kupita kwenye bomba za maji safi.

(b) Je, lini Kampuni ya Rand Water itatenganisha chemba za maji machafu na maji safi katika eneo la Mji Mkongwe.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

179. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Awamu ya Nane inaendelea kufanya kazi nzuri ya kujenga skuli za kisasa. Hata hivyo, kufuatia ziara za kusikiliza maoni na changamoto za wananachi wa hapo, imebainika kuwa, kuna eneo zuri liliopo karibu na Skuli ya Shidi Msingi, linalouzwa kwa shilingi milioni kumi za Kitanzania (Tsh. 10,000,000) lakini wananchi hao hawana uwezo wakulipia gharama hizo.

(a) Ni lini Serikali itawaunga mkono wananchi hao kwa kutoa kiasi hicho cha fedha na kulinunua eneo hilo.

(b) Ni lini Serikali itaijenga Skuli ya Shidi Msingi ili nayo iwe na majengo ya kisasa.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

113. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Barabara ya Mchanga-kwale pembeni ambayo ipo katika jimbo la Ziwani haipo katika hali nzuri ambapo kina mama wengi wanaitumia barabara hii kwa shughuli zao za kujitafutia riziki kwa wajasiriamali ambao wanabeba udongo kwa kichwa kwa ajili ya kutengeneza vyungu karibu na barabara hiyo ikijengwa itawarahisishia katika harakati zao.

Je, lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

171. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Kwa kuwa katika barabara ya Melitano hadi Wete imepita Jimbo la Ziwani, na kwa kuwa kuna ujenzi wa mitaro yenye kina cha mita moja kwenda chini ambayo ipo katika makaazi ya watu wenye hali tofauti na haikuwekewa vizuizi wala mifuniko.

(a) Kwanini Serikali haioni kuwa kutowekewa vizuizi mitaro hiyo kunahatarisha maisha na usalama wa watoto na Watu Wenye Ulemavu.

(b) Je, lini Serikali itachukua juhudi za dharura za kuziba mitaro hiyo.

255. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Mnara wa Kigomasha ni kati ya minara ambayo ina historia na ilikuwa inaongozea vyombo vilivyokuwa vinatoka nchi mbalimbali duniani.

Kwa kiasi gani Wizara yako inaitambua na kuitambulisha kwa wengine, historia ya mnara huu.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

122. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Imebainika kuwa asilimia kubwa ya mazao ya kilimo yanayotumika Zanzibar yanatoka Tanzania Bara.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha sekta ya kilimo na kuhakikisha wakulima wa Zanzibar wanazalisha mazao yatakayotosheleza kutumika Zanzibar na mengine kusafirishwa nje ya Zanzibar.

157. MHESHIMIWA MOZA MOHAMMED KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mifugo ya kuku ni kitoweo ambacho watu wengi wa Zanzibar wanakitegemea kama ni chakula katika maisha yao ambapo takriban Makasha (Containers) tano mpaka kumi zinauzwa kwa Zanzibar kwa matumizi ya kila siku.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kilimo cha kuku kinaimarishwa ili wananchi waweze kumudu kununua kuku kwa bei ya chini na ikiwezekana kufuga wenyewe.

**Wizara ya Afya:**

164. MHESHIMIWA MASOUD AMOUR MASOUD (Jimbo la Amani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu katika sekta ya afya.

Ni lini sasa Serikali itaimarisha huduma za mashine za kidigitali za *X-ray* na *Ultrasound* katika kituo cha afya cha Wazee, ili kusaidia kupunguza msongamano katika hospitali za Wilaya.

194. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kitengo cha Tiba ya Viungo (*Physiotherapy*) katika Kituo cha Afya cha Chake Chake, kinatumia baadhi ya vifaa vya muda mrefu ambavyo haviendani na mahitaji ya sasa ya huduma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia kitengo hicho vifaa vipya na vya kisasa, ili kuboresha ubora na ufanisi wa huduma za tiba ya viungo.

274. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Kwa kiasi gani Serikali imepunguza gharama za matibabu baada ya Hospitali za Umma kuwapa wawekezaji.

(b) Kwa kuwa malalamiko ya hospitali hizo kupewa wawekezaji yameongezeka, je, Serikali inaweza kuwaambia wananchi, ni hasara na maslahi yepi yamepatikana kabla na baada ya Hospitali za Umma nchini kupewa wawekezaji.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya habari na Ubunifu:**

188. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Serikali imewekeza katika mifumo mbalimbali ya TEHAMA, ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za umma.

(a) Je, ni mifumo mingapi ya Serikali inayosimamiwa na kuendeshwa kikamilifu na wataalamu wa Serikali bila ya kutegemea kampuni binafsi (vendors).

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wataalamu wetu wa ndani kuweza kutengeneza mifumo moja kwa moja.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

241. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Sheria ya Ajira ya Zanzibar, Nam. 11 ya 2005, ni Sheria inosimamia viwango vya kazi kwa Zanzibar katika kuhakikisha kwamba haki za wafanyakazi zinalindwa. Hata hivyo, Sheria hiyo ni ya muda mrefu na haiendani na wakati uliopo, kwa kuwa baadhi ya vifungu vyake haviwezi kuendelea kuwalinda wafanyakazi na pia katika kusimamia utekelezwaji wake ina miaka 21 tokea kutungwa kwake.

Je, Wizara yako imezichukua hatua zipi kuhakikisha kuwa inaifanyia mapitio Sheria hiyo.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari kwa ajili ya Kusimamia, Kuendeleza Uvuvi na Kuhifadhi Maliasili za Bahari na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
15 Septemba, 2026.

(Ramadhan Khamis Juma)
KAIMU KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR